Sitiari Zinavyoendeleza Mfumodume Katika Ndoa Miongoni Mwa Abagusii

Cecilia F. Gekong'a
Laikipia University, Kenya

Abstract

Human thoughts are depicted through communication. This is done through deliberately chosen words and utterances as expressions of specific purposes. The Abagusii community teachings and guidance are delivered to varied audiences, with intentions of educating, warning, advising and coercing its members about the societal obligations and values. The study is an investigation of male chauvinism among the Abagusii which leads to gendered social relations. This situation is brought about by social systems that uphold man above woman in society right from childhood. For a long time, the aspect of male chauvinism has been nurtured and propagated in this society. At the onset of marriage, specific pre-marital instructions and teachings are undertaken to cement this in form of advice given to the bride and groom. This was an area that had not been adequately studied. The main objective of this study was to investigate how the use of metaphors in advice to bride and groom in this century is a great contribution to male dominance in the society. Metaphors were investigated due to the fact that they play a key role during advice and guidance. The study was guided by African Feminism Theory. This is because of its demand to bring about changes in approaches that look down upon women. Critical Discourse Analysis Theory was also used to unearth the gendered power relations and how they are portrayed through the use of language. This was a field study whereby data was collected through interviews, observation and field notes. The findings of the study established that a woman is given an inferior identity and gendered roles, which portray her as weak in the society that values male chauvinism. The study will of great contribution to oral literature. It will also show how this discrimination hinders some millennium goals like gender equality.

Keywords: Advice, feminism, gendered power relations, patriarchy, metaphors.

Ikisiri

Mawazo ya binadamu hudhihirika katika mawasiliano, kupitia kwa maneno yaliyoteuliwa kiufundi na kutumika kwa malengo maalum. Mawaidha miongoni mwa Abagusii hutokea katika miktadha mbalimbali ya kijamii na yanalenga hadhira kwa nia ya kuelimisha, kuonya, kushauri na kushawishi. Swala katika utafiti huu ni kuwa katika jamii ya Abagusii, mwanamume huwa na mamlaka ya juu kuliko mwanamke. Hali hii imesababishwa na mfumo wa kijamii ambao hutukuza wanaume tangu utotoni hadi utu uzima. Kwa muda mrefu, swala la mfumodume kukuzwa, kuhalalishwa na kuendelezwa katika ndoa limedhihirika kupitia kwa mawaidha wanayopewa maharusi. Hata hivyo, swala hili halijafanyiwa uchunguzi wa moja kwa moja katika nyanja ya fasihi simulizi. Lengo kuu la makala hii ni kuchunguza jinsi sitiari zinazotumika katika mawaidha kwa maharusi katika karne hii zinavyoendeleza na kudumisha mfumodume katika jamii. Sitiari ndizo zilizingatiwa na kuchunguzwa kwa sababu zina nafasi kubwa katika mawaidha. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ilielekeza utafiti huu kutokana na msukumo wake wa kujaribu kuleta mabadiliko katika mitazamo ya kijinsia inayomkandamiza mwanamke. Vilevile, nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi ilisaidia kuangazia mahusiano ya mamlaka ya kimenke yanavyoendelezwa kupitia kwa matumizi ya lugha. Utafiti huu ulifanyika nyanjani ambapo deta ilikusanywa kupitia kwa njia ya uchunguzi na mahojiano. Utafiti huu ulibainisha kwamba mwanamke amepewa utambulisho na majukumu ya kimenke ambayo humsawiri kuwa duni na dhaifu katika utamaduni unaoenzi mfumodume. Makala hii itakuwa mchango adhimu katika nyanja ya fasihi kwa jumla. Aidha itaonyesha jinsi ubaguzi huu unavyochangia kutofikia baadhi ya malengo ya milenia kama

vile usawa wa jinsia. Mawaidha kwa maharusi ni uwanda ambao unahitaji ufanyiwe tafiti zaidi za kitaaluma kwa sababu ya majukumu yake kwa jamii.

Maneno muhimu: Mahusiano ya mamlaka ya kimenke, mawaidha, mfumodume, sitiari, ufeministi.

Utangulizi

Kama jamii zingine kote ulimwenguni, jamii ya Abagusii hutambulishwa na itikadi zinazotumiwa kuongoza maisha ya watu. Itikadi hizi kama vile mfumodume hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kupitia asasi mbalimbali za jamii mojawapo ikiwa ni ndoa.Tangu jadi, jamii hii ya Abagusii imekuwa ikikweza wanaume na kutweza wanawake kupitia kwa majukumu mbalimbali ya kimenke wanayopewa wanawake na wanaume katika ndoa. Hali hii ya mahusiano ya mamlaka ya kimenke imerejelewa kupitia kwa mbinu za lugha zinazotumika katika mawaidha wanayopewa maharusi siku ya harusi. Huu ni muktadha maalum unaoruhusu hotuba mbalimbali huku mawaidha yakiwa kilele cha mazungumzo ya hafla hii. Aidha, mbinu za lugha zinazotumika katika mawaidha huwa za kiufundi na zilizo na uwezo mkubwa wa kuathiri mitazamo ya maisha ya maharusi. Hata hivyo, ikumbukwe kuwa msingi wa mawaidha haya kwa maharusi ni kufunza, kuelekeza na kushawishi wala si kutisha au kuogofya.

Mfumodume ni ile hali ya mwanamume kuwa mwenye uamuzi katika uhusiano hasa wa kifamilia. Ni hali ambapo mke hana usemi mbele ya mumewe. Millet (1978) anaeleza kuwa mfumodume katika jamii umejikita katika ngazi za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Mfumo huu huathiri wanaochukuliwa kuwa dhaifu katika jamii na hivyo kuchangia mahusiano ya mamlaka ya kimenke kati ya wanaodhulumu na wanaodhulumiwa. Hali inayokweza mfumodume inayorejelewa katika mawaidha kwa maharusi inachangia katika mielekeo ya hivi sasa ya ndoa katika jamii ya Abagusii. Kutokana na mawaidha haya, inadhihirika kuwa mke mwema katika ndoa ni yule anayefuata na kuzingatia ushauri na maaso anayopewa. Katika ile hali ya kudumisha mahitaji haya, mke anaishia kujiingiza katika hali inayomtenga na kumfanya aonekane kama kiumbe duni akilinganishwa na mume katika ndoa. Mwelekeo huu unamfanya mwanamke katika jamii ya Abagusii kuchukua sura halisi ya mke wa kiafrika kwa mujibu wa ufeministi wa kiafrika ambao unapinga tamaduni zinazomkandamiza mwanamke katika jamii (Rutere, 2009). Ni katika muktadha wa mawaidha haya ambapo mwanamke katika jamii hii, anaelekezwa na tamaduni na hapa ndipo usuli huu umeibua mada hii kuhusu mawaidha harusini yanavyomdunisha mwanamke katika ndoa.

Utafiti huu ulichunguza jinsi matumizi ya sitiari katika mawaidha yanavyoenzi mfumodume na kudunisha mwanamke katika ndoa na hivyo kudumisha hali hii inayomnyima mwanamke nafasi ya kujiendeleza katika ngazi zote za kijamii. Uchunguzi huu wa sitiari ulionyesha mielekeo ya jamii kuhusu wanawake. Kati ya mielekeo inayojitokeza katika sitiari hizi ni kuwa lugha inayosawiri wanawake ni ya kuwadunisha. Kupitia kwa wanajamii wenyewe wanaoendelea kushikilia mtazamo huu, wanadhihirisha kuwa wanasaidia kudumisha hali inayokweza wanaume na kudhibiti wanawake.

Kwa mujibu wa *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (TUKI, 1990), sitiari ni mtindo wa usemaji ambao hulinganisha vitu au watu bila kutumia viunganishi. Hivyo, ni dhahiri kuwa matumizi ya sitiari hayawi ya kiholela au msemaji halinganishi vitu viwili kiistiari kwa sababu ya kuvilinganisha tu, bali ni lazima kuwe na dhamira au lengo fulani la huo ulinganishi. Dhamira hiyo ndiyo hasa humfanya mzungumzaji aamue ni sitiari ipi atatumia na hivyo ni dhahiri kuwa matumizi yoyote yale ya sitiari hulengwa kwenye hadhira husika. Mwosha (2011) alitafiti matumizi ya lugha katika sherehe za kumfunda mwari miongoni mwa Wazaramo nchini Tanzania. Kati ya kunga za lugha alizozingatia ni sitiari. Utafiti wake

ulibaini kuwa sitiari hubeba ujumbe mzito kwa mwari na jamii kwa jumla na hivyo humsaidia mwari kupata ujumbe uliokusudiwa kwa njia fupi na kufanya unate vizuri akilini.

Nadharia za Ufeministi na Uchanganuzi Hakiki wa Usemi

Utafiti huu unategemea ufeministi wa eneo la Afrika. Nadharia hii inaangazia jinsi miktadha tofauti ya kijamii inavyochangia unyanyasaji na udunishaji wa mwanamke katika jamii. Steady (1981) anashikilia kuwa Nadharia ya Ufeministi ndiyo inafaa kuchunguza hali za kijamii na kitamaduni zinazorutubisha unyanyasaji wa mwanamke katika jamii.

Kama anavyoeleza Otiso (2016) umenke katika jamii ya Abagusii ni hali ambayo huzingatiwa kuanzia wakati mtoto anaanza kujifunza lugha. Ni katika hii lugha ambapo vipengele vya jinsia na umenke vimeambatanishwa kupitia kwa mbinu mbalimbali kama vile misemo na sitiari. Mwanamke katika jamii nyingi za Kiafrika amesawiriwa kama kiumbe dhaifu na ametengewa nafasi inayoonekana kuwa ni ya chini lakini iliyo na majukumu mengi ikilinganishwa na yale ya mwanamume. Kwa msingi huu, inabainika kwamba mwanamke ambaye anathamini ndoa yake na watoto atakubali kudhulumiwa na mumewe kwa vyovyote vile ili kudumisha ndoa yake. Hata hivyo, Betty (1977) anashinikiza wanawake wasikubali hali hii inayowakandamiza na kuwafungia katika maeneo ya nyumbani bali wasimame wima katika mstari wa mbele na kuchukua majukumu katika mawanda mbalimbali ya umma. Mawazo haya ni sawa na maoni ya Wamitila (2003) kwamba nadharia ya ufeministi imewekewa msingi na msukumo mkubwa pamoja na nia ya kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kitamaduni, kidini, kijamii, kisiasa na kiuchumi. Hizi ni pingu ambazo zimejengeka katika msimamo na itikadi za mfumodume. Kama inavyojitokeza kupitia kwa sitiari katika mawaidha harusini, kudhulumiwa kwa mwanamke kumerutubishwa na mfumodume unaomuenzi mwanamume na kumtweza mwanamke.Ufeministi huishambulia mitazamo ya kiume kuhusu jinsi mwanamke anavyopaswa kuishi, kufikiri na kuitikia katika hali mbalimbali za kimaisha.

Kwa jumla nadharia hii ya Ufeministi wa Kiafrika inajaribu kuleta mabadiliko katika mitazamo ya kijinsia inayomkandamiza mwanamke na kutishia hali yake ya kijamii na kibinadamu. Hivyo tatizo la mwanamke litasuluhishwa tu iwapo haki na nafasi sawa itatolewa kwa wanawake kama ilivyo kwa wanaume. Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi, Fairclough (1992) ilisaidia kuangazia na kufichua masuala muhimu ya jamii kama vile mahusiano ya mamlaka ya kimenke kati ya wanajamii. Kwa mujibu wa misingi ya nadharia hii, lugha ni tendo la kijamii, van Dijk (1999) anaunga mkono suala hili kwa kusema ni kupitia kwa lugha ambapo ulimwengu husawiriwa. Hii ni kwa sababu usemi wowote na matumizi ya usemi huo huundwa na jamii na hivyo uchanganuzi wa usemi hauwezi kutengwa na jamii husika, bali uangazie matendo ya kijamii na masuala ya itikadi yanayozunguka matini. Kwa mujibu wa nadharia hii, mhimili huu uliwezesha mtafiti kuchanganua sitiari katika mawaidha harusini na kupata maana fiche inayohusishwa na matini.

Mbinu za Utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika kaunti za Nyamira na Kisii mkoani Nyanza wanamoishi wanajamii wa Abagusii. Eneo hili lilitumika kuwakilisha jamii pana ya Abagusii popote walipo nchini Kenya. Jamii hii hushiriki katika sherehe mbalimbali za kijamii ambapo harusi ni mojawapo. Lugha wanayoitumia wanajamii ni Ekegusii ambayo inabeba vipengele vinavyohusiana na maisha ya jamii hii. Utafiti huu uliangazia sitiari katika mawaidha na kuona mchango wake katika kudunisha mwanamke, hali ambayo inachangia kuendeleza mfumodume katika jamii hii.

Uteuzi uliofanywa hapa ulikuwa wa kimakusudi ili kutimiza madhumuni ya utafiti. Mtafiti aliteua sherehe tano za harusi alizohudhuria huku akiacha zile ambazo zilifungwa

katika ofisi ya mkuu wa kaunti. Hii ni kwa sababu hazifuati utaratibu wa kutoa nafasi ya mawaidha kulingana na utamaduni wa jamii ya Abagusii. Kati ya sherehe alizohudhuria mtafiti ni zile ambazo alialikwa na zingine aliandamana na jamaa au rafiki aliyealikwa. Sherehe alizohudhuria ni zile ambazo bwana na bibi harusi ni wa kutoka jamii ya Abagusii kwa sababu harusi ile inahusishwa na utamaduni wa jamii hii.

Njia zilizotumika katika ukusanyaji wa deta ni mbili. Kwanza njia ya uchunguzi ilitumika ambapo mtafiti alihudhuria sherehe za harusi kwa nia ya kupata sitiari katika mawaidha yanayoendeleza umenke katika jamii ya Abagusii. Deta pia ilikusanywa kwa kutumia mbinu ya mahojiano kwa nia ya kupata maoni ya wasailiwa kuhusu mada ya utafiti. Ili kufikia wasailiwa, mtafiti alitumia mfumo wa mtandao wa kijamii ambapo alielekezwa na wanajamii kwa watu ambao wamepitia sherehe hii ama wale ambao wamewahi kutoa mawaidha kwa maharusi. Sampuli iliyopatikana ilikisiwa kuwa ingeweza kuwakilisha jamii nzima ya Abagusii. Hii ni kwa sababu kundi ndogo la sampuli humwezesha mtafiti kupata habari za kina kuhusiana na mada ya utafiti (Milroy, 1987). Katika utafiti huu mtafiti alitumia mbinu ya kithamano ili aweze kuelezea kwa undani matokeo ya utafiti. Katika uchanganuzi wa deta, mtafiti aliweza kuweka deta iliyorekodiwa katika maandishi. Deta iliyokuwa katika lugha ya Ekegusii ilitafsiriwa hadi lugha ya Kiswahili kwa kutumia tafsiri ya kisemantiki ili kudumisha maana ya matini kama ilivyokusudiwa na mzungumzaji. Ili kufikia malengo ya utafiti, deta ilipangwa kwa utaratibu ambao ulirahisisha uchanganuzi.

Uchanganuzi na Matokeo ya Utafiti

Deta zilizokusanywa zimewasilishwa kwa njia ya maelezo. Haya maelezo yamezingatia sitiari katika mawaidha kwa maharusi. Maelezo yamehusisha fasiri na umuhimu wa sitiari hizi kwa wanandoa huku lengo la utafiti likizingatiwa. Uchanganuzi wa sitiari katika mawaidha harusini miongoni mwa Abagusii umeonyesha mielekeo ya jamii kuhusu mwanamke na nafasi anayotengewa katika jamii. Inabainika kupitia kwa mielekeo hii kwamba sitiari hizi humsawiri mwanamke kwa njia inayomdunisha. Hii ni kwa sababu utamaduni ni muhimu katika kumfunza mtoto au mtu mzima itikadi za jamii. Mawazo mengine yanayochangia kuhusu umuhimu wa utamaduni katika kukuza lugha ya mtu, yanaonyesha kwamba kupitia kwa lugha ndipo tunajifunza kuhusu jamii zetu na kushiriki katika shughuli za kijamii kama inavyopasa. Ni bayana kuwa kila mtu hutoka katika jamii iliyo na miundo mbalimbali inayotumiwa kugawanya watu kwa misingi mbalimbali, kama vile ya jinsia na umenke. Katika utafiti huu mgawanyiko huu unajibainisha kupitia kwa sitiari zinazotumiwa katika mawaidha harusini.

Sitiari hulinganisha vitu ama watu lakini bila kutumia viunganishi linganishi vya mithili ya, mfano wa, sawa na, kama na vinginevyo (Senkoro, 1982). Naye Ndumbu (2013) amefafanua sitiari kama neno lililozaliwa kutoka kwa neno sitiri. Kusitiri ni kuficha au kufunika. Hii inamaanisha, kuwa maana ya msingi ya kitu ambacho hutajwa, hukiukwa na hivyo maana inayorejelewa huwa ni ya pragmatiki. Matumizi ya sitiari ni njia muhimu inayotumiwa ili kurejelea mwanamume na mwanamke katika jamii. Sitiari hizi zinabaini taswira mbalimbali ambazo mwanamke na mwanamume wamepewa katika jamii pamoja na majukumu yao ya kimenke. Katika mawaidha harusini, sitiari kadhaa zinatumika kuwakilisha majukumu ya kijamii wanayostahili kuchukua wanandoa.

Mifano ya Sitiari Zilizoshughulikiwa

Omosacha nere ritiro rienyomba
Mwanamume ndiye mhimili katika nyumba

Katika mawaidha haya, sitiari mhimili inatumika kuashiria mwanamume aliyeoa na ana familia yake katika jamii ya Abagusii. Mhimili au nguzo ni ule mti ambao huwekwa katikati ya nyumba ya kienyeji inapojengwa ili kuifanya iwe imara. Mhimili huu huenda hadi kwenye paa kisha mnara unawekwa upande wa nje. Mwanamume hapa anafananishwa na mhimili kwa vile kuwepo kwake kutaifanya familia yake iwe imara na atailinda kunapotokea tatizo lolote.Vilevile mwanamume ndiye mwamuzi katika kila jambo linalohusiana na familia yake. Kama anavyoeleza Nyang'era (1999), mume ambaye ni nguzo katika familia afapo, ule mnara huondolewa kuashiria nyumba hiyo haina mhimili. Analojia hii ya mhimili imetumika kuonyesha mamlaka ambayo mwanamume hupewa katika jamii ya mfumodume na ndiposa anastahili kuheshimiwa. Riro (2006) amebaini kuwa katika jamii ya Abakuria, mwanamume amepewa sura ya uyoga inayomsawiri kama nguzo ya familia. Anafananisha ule mhimili wa uyoga na hali halisi ambapo ni lazima mwanamume adhihirishe anayopaswa kufanya kama vile kulinda na kuitosheleza familia yake. Hata hivyo, kuna msemo unaopatikana katika lugha ya Kiingereza kuwa 'Nyuma ya kila mwanamume anayefaulu maishani kuna mwanamke'. Msemo huu ni kinyume na itikadi ya jamii ya Abagusii. Hii ni kwa sababu ufanisi wote katika jamii au familia unahusishwa na mwanamume. Kama anavyoeleza Levine (1980), kila boma lina baba anayerejelewa kama 'mwenyewe' na ndiye anayeelekeza mambo katika boma. Katika jamii hii mwanamume aliruhusiwa kuoa wanawake wengi ambapo alikuwa kiongozi na nguzo katika kila boma.

Omokungu nere enyomba
Mwanamke ndiye nyumba

Katika jamii hii inayoenzi mfumodume, mwanamke analinganishwa na nyumba. Tangu jadi mwanamke alikuwa akipewa majukumu ambayo yalimfunga katika mazingira ya nyumbani. Kupitia kwa sitiari nyumba, wazungumzaji katika mawaidha wanajaribu kuonyesha mambo muhimu yanayohusishwa na majukumu au maeneo ya pale nyumbani, kwa sababu nyumba inahitaji mwanamke ili aweze kupika, kusafisha na kulea watoto. Kwa hivyo, bila mke hakuna nyumba. Katika muktadha wa ndoa, uzao wa mwanamume kupitia kwa mkewe unarejelewa kama nyumba. Sitiari hii inabeba taswira ya familia iliyo na mke na watoto. Mwanamume anapotaja idadi ya nyumba alizonazo ama anazomiliki inamaanisha idadi ya wake zake. Mwanamume hapa amepewa hadhi ya juu kutokana na hali yake ya kumiliki nyumba ambayo inahusisha mwanamke na watoto atakaozaa. Katika mawaidha haya vilevile mwanamume alishauriwa kuwa:

Rero kwanyorire mwao
Leo umepata kwako

Sitiari katika usemi huu imetumika kwa njia ambayo inamfanya mwanamke awe kama mali ya mwanamume. Sitiari ya neno kwako inasimamia mke. Mke katika muktadha huu amepewa mamlaka ya pale nyumbani na majukumu yanayomfunga katika mazingira hayo kama vile kulea watoto, kupika na kumtumikia mumewe anapofika nyumbani. Katika mazungumzo ya kawaida mwanamume humrejelea mkewe kama nyumba yake. Urejeleo huu humsawiri mwanamke kama chombo ambacho ni cha kutumiwa na mumewe kwa ajili ya kujiliwaza na kujipooza baada ya shughuli zake za siku.

Enda nero amaebi
Tumbo ndiyo dawa ya mapenzi

Dawa ya mapenzi huaminika kuwa ni kitu anachopewa mtu ili ampende yule aliyempa dawa hiyo (fasiri yetu). Kulingana na mawaidha ambayo bibi harusi anapewa, anashauriwa kuwa akitaka mume wake ampende, ni sharti amlinde vyema kwa kumpikia chakula kitamu. Kupitia kwa sitiari hii, dawa inayopendekezwa ni kule kumpikia mumewe. Hapa inadhihirika kuwa mwanamke ana uwezo wa kumfanya mumewe ampende kwa kutumia nafasi aliyopewa kulingana na jukumu la kimenke la kuwa mpishi mwema. Kwa mujibu wa sitiari hii, ni wajibu wa mwanamke kukidhi mahitaji ya mume wake kwa kumpikia chakula kitamu kutokana na ujuzi wa upishi. Kwa kufanya hivi, atakuwa amemteka bakunja mumewe. Msisitizo unaowekwa hapa ni ule wa kumfunga mwanamke katika maeneo ya nyumbani akizingatia majukumu aliyopewa. Mwanamke hapa amenyimwa uhuru wa kutekeleza majukumu mengine yatakayomfanya atoke nyumbani ambayo huchukuliwa kuwa himaya ya mwanamume. Katika muktadha huu, mwanamke pia anonywa kuwa asipompikia mumewe chakula kizuri, huenda mumewe asimpende na mwishowe atatoroka akaoe mke mwingine.

Rero etaya yokire
Leo taa imewaka

Kutokana na mawaidha wanayopewa maharusi, mwanamume anaambiwa kuwa leo taa imewaka kwake. Sitiari hii imetumiwa ili kumfananisha bibi harusi na taa ama mwangaza. Mwanamke anapongezwa kwa vile ameolewa na atakuwa faida kwa jamii ya mumewe. Ufananisho huu unamfanya mwanamke aelekezwe kwenye majukumu yake ya nyumbani kama vile kunadhifisha nyumba, kupika, kulea watoto, kulima na kumtumikia mumewe. Mafanikio ya mwanamke katika kutekeleza majukumu ya kimenke ndiyo yanaashiriwa kama nuru inayotoka kwenye taa.

Twakoire omwana amaridadi
Tumekupa mtoto maridadi

Katika mawaidha aliyopewa bwana harusi, anaambiwa kuwa amepewa mtoto maridadi. Bibi harusi hapa ndiye anarejelewa kama maridadi au pambo. Umaridadi huu unatokana na urembo wa mwanamke asiye na doa. Taswira hii ya mwanamke kama pambo ina maana ya uzuri wa umbo la mwanamke linalotumika ili kumfurahisha mwanamume. Kama anavyoeleza Momanyi (2001), maumbo haya ya lugha hushehenezwa kwenye nafsi ya kike na kujenga ubandia wa nafsi. Mwanamke huweza kujichukua kama pambo tu la kumfurahisha mwanamume, na kwa hivyo kugubikwa ule uwezekano wa yeye kujifikiria kama kiumbe mkamilifu anayeweza kufanya mengi maishani badala ya kuwa pambo tu. Ni katika muktadha huu ambapo mwanamume anapewa jukumu la kumlinda mwanamke ili aweze kudumisha ule urembo au umaridadi wake. Maaso anayopewa ni kuwa asimdekeze mkewe kwa kutokidhi mahitaji yake. Inabainika hapa kuwa mwanamke anamtegemea mumewe ashughulikie ule urembo wake kwa kumpa kila anachohitaji ili aendelee kumpendeza. Vilevile kupitia sitiari hii, mwanamume anaonywa asimfanyie mkewe matendo ambayo yatamaliza ule urembo au umaridadi wake.

Omari, Mkomwa na Mlingi (2016) wanaeleza kuwa katika jamii ya Waswahili mwanamume anastahili kumpamba mkewe kwa mavazi yanayopendeza. Katika uchunguzi wao kupitia kwa maandishi ya makawa na vipepeo, misemo iliyojitokeza ni kama:

Kupamba mke ni sifa ya mume
Mke ni nguo mgomba kupalilia
Usione utamu wa ndizi mgomba wataka palizi
Mke ni tunda wajibu kumtunza

Misemo hii yote inaonyesha mwanamke anastahili kupewa kila anachohitaji ili aendelee kupendeza hasa machoni mwa mumewe. Hata kama mwanamke atajishughulikia na kujitunza, bado ile dhana ya mume kumtunza mkewe inashikiliwa katika jamii kama jambo la lazima. Hali hii ya kumfanya mwanamke kumtegemea mumewe huweza kumfanya mwanamke kuwa kiumbe dhaifu anayengoja kutunzwa na hivyo kuwa chini ya mumewe ambaye ndiye mwenye mamlaka katika familia.

Orande buna emanga na esameta
Uenee kama mlima Manga na mlima Sameta

Katika hotuba ya mmoja wa wazungumzaji, bwana harusi aliombewa baraka ili aenee kama mlima Manga na mlima Sameta. Katika jamii ya Abagusii, milima hii huwa imesifika sana kutokana na jinsi ilivyoenea. Mwanamume anapoambiwa aenee inamaanisha azae watoto ili kuendeleza jamii. Uwezo wa kuwa na familia ni jambo lililopewa uzito hivi kwamba kuwa na watoto wengi, wasichana na wavulana ilikuwa ni sifa kubwa kwa mwanamume na iliyompa hadhi katika jamii yake. Sitiari ya kuenea kama hii milima ni sawa na kupanua nasaba ya jamii kwa jumla. Kama anavyoeleza Nyang'era (1999), mwanamume anapewa hadhi katika jamii anapobarikiwa na watoto hasa wa kiume kwa vile ukoo wake utaendelea. Aidha angekuwa na uwezo wa kupata mali kutokana na watoto wake na kuwa wa kujitegemea. Kuenea kwake kulishirikisha hata wakwe zake. Hata hivyo, iwapo mwanamke hakuzaa watoto hasa wa jinsia ya kiume, mumewe alikuwa na uhuru wa kuoa wanawake wengine ili wamzalie watoto wa kiume. Kulingana na Aberi na Yieke (2009), wavulana tu ndio walioruhusiwa kurithi mali ya familia hasa shamba kwa sababu jamii hii inaongozwa na misingi ya mfumodume. Utamaduni huu unaongozwa na mielekeo kuwa wanaume ndio wana uwezo wa kuendeleza jina la ukoo kwa vile wanawake huolewa na kuwa mali ya mume.

Twakoire omwana omuya
Tumekupa mtoto mzuri

Kulingana na utamaduni wa jamii ya Abagusii, msichana alipashwa tohara ili kuingia utu uzima. Kabla ya kitendo hiki alirejelewa kama mtoto. Hata hivyo sitiari 'omwana' imetumika kwa njia tofauti katika muktadha huu. Maana iliyofichika katika neno hili ni kuwa bibi harusi ni mtoto kwa sababu hana tajriba yoyote katika maisha ya unyumba. Mama yake bibi harusi anatumia sitiari hii kuonyesha uzuri wa msichana huyu ambaye hana dosari yoyote bali anastahili kulindwa. Kulingana na tamko hili mwanamke bado anawekwa katika ile sehemu ya chini akilinganishwa na mwanamume ambaye anasawiriwa kama mwenye nguvu na anayestahili kumlinda msichana. Katika muktadha huu bibi harusi pia alirejelewa kama 'rige' yaani kinda. Kama anavyoeleza Otiso (2016), kinda hana ujuzi wowote maishani bali anastahili kufunzwa jinsi ya kuishi. Vilevile, kukua kwake kunategemea ulinzi atakaopewa na mumewe. Kwa hivyo mwanamume anapewa mamlaka ya kumfunza mkewe jinsi anavyotaka. Hali hii inaonyesha mwanamke katika ndoa hana usemi wowote wala uwezo wa kushughulikia mambo au maswala mbalimbali bali humtegemea mumewe ampe mwelekeo. Kama mtoto mdogo, hana uwezo wa kujihudumia isipokuwa kupata huduma kutoka kwa wenye uwezo kama vile mama yake ambaye sasa anapitisha jukumu hilo kwa mumewe. Hivyo mume anakumbushwa jukumu lake la kutafuta mali ili kukimu mahitaji ya mkewe. Vilevile, anatarajiwa amlinde na kumkinga kutokana na utesi wowote au mambo yoyote mabaya kutoka kwa jamii.

Omoiseke ensobosobo

Msichana zabibubata

Katika mawaidha kwa wanandoa, zabibubata ambalo ni tunda ni sitiari ya kijazanda inayotumiwa kumrejelea bi harusi. Mwosha (2011) anadai tunda kawaida huwepo kwa ajili ya kuliwa. Anaeleza kuwa jamii ya Wazaramo nchini Tanzania, huamini kwamba mwanamume ndiye hujisikia kula tunda (kushiriki katika kitendo cha ndoa). Mwanamke naye ni tunda ambalo lipo kwa ajili ya kuliwa na mwanamume. Maoni haya yanalingana na ya Onchoke (2017) kuwa mwanamke husawiriwa kama tunda tamu linaloliwa. Hata hivyo si matunda yote yalitumiwa kumsawiri mwanamke bali yale yaliyo na sifa za kuwa na harufu inayopendeza na utamu au sukari. Kulingana na ufananisho katika muktadha huu, tunda lililotumika kumrejelea bibi harusi ni zabibubata kwa sababu ya sifa zake za kuwa na rangi ya chungwa linapoiva, utamu wake na vilevile umbo lake la mviringo. Sitiari hii ilitumika kwa vile katika jamii hii, weupe wa msichana ni sifa moja ya kuwa mrembo na hivyo mwanamke hapa alichukuliwa kuwa ameiva na yuko tayari kuolewa ili kumburudisha mumewe kutokana na ule ubivu wake. Ni katika msingi huu ambapo ilibainika kuwa mwanamume alimchukua mwanamke kama chombo cha kumfurahisha. Utamu wa tunda hili pia unaweza kulinganishwa na maneno matamu ya bibi harusi ambayo ni ya kuleta amani, na vilevile kuburudisha hasa kwa mumewe. Waandishi kama Omari, Mkomwa na Mlingi (2016) walichunguza sauti za wanawake nchini Tanzania kupitia kwa maandishi katika makawa na vipepeo. Hivi ni vifaa vya nyumbani ambavyo aghalabu wanandoa hupewa siku ya harusi. Kati ya maandishi katika vifaa hivi ni kama: *Ni zako zabibu kula taratibu* na *kula polepole nanasi hili ni lako.* Kupitia kwa sitiari hizi za matunda, mwanamke amejifananisha na tunda ambalo linaliwa na wanaume. Hali hii ya kumsawiri mwanamke kama chakula inampa hadhi ya chini inaonyesha yuko tayari kwa kila hali kumtimizia mumewe haja zake na kumfurahisha.

Omosacha nere enyimbo
Mwanamume ndiye fimbo

Fimbo ni sitiari ambayo inafananishwa na mwanamume katika ndoa. Mwanamke anapoolewa, mumewe anakuwa kama fimbo yake ya kutembelea. Mwanamke anawacha kutumia jina lake na anaanza kurejelewa kwa jina la mumewe (mke wa). Katika jamii, mwanamke huyu ataheshimiwa na atapata hadhi kutokana na kuwa mke wa mtu. Hali ya kujitambulisha kwa jina la mumewe ni kuonyesha nafasi ya chini anayopewa mwanamke katika jamii. Anategemea utambulisho unaohusishwa na mumewe ili aweze kusikika na kutambuliwa katika jamii.

Omogaka nere omotwe ase omochie
Mwanamume ndiye kichwa katika boma

Katika mawaidha yanayolenga maharusi, kichwa ni sitiari inayotumiwa kusawiri uwezo na mamlaka aliyopewa mwanamume. Sitiari hii inamfananisha mwanamume na kichwa, kwani kichwa ndicho kinabeba akili inayohitajika katika kufikiria na pia macho yanayohitaji kuona. Hivyo basi mwanamume kufananishwa na kichwa, tunapata kuelewa kwamba ni mwenye hekima inayohitajika katika kuongoza familia yake. Kulingana na Aberi na Yieke (2009), tangu jadi nafasi ya uongozi katika jamii hii iliachiwa wanaume. Mume ndiye kiongozi wa familia huku mke na watoto wakiwa chini ya uongozi wake. Kulingana na maelezo ya wasailiwa, kuna mambo ambayo mwanamke hawezi kufanya bila kupata idhini kutoka kwa mumewe ambaye ndiye kichwa cha familia. Majukumu ambayo hastahili kutenda

ni kama vile kuuza ng'ombe ama kuchukua mahari ya bintiye. Mwanamke anaruhusiwa kuuza kuku, mayai na maziwa, bidhaa ambazo zina faida ndogo.

Hitimisho

Uchanganuzi huu wa sitiari katika mawaidha harusini uliweza kubaini kuwa mahusiano ya mamlaka ya kimenke katika jamii huwa yameambatanishwa na itikadi ambazo zimewekwa na jamii inayopendelea mfumodume. Hali hii huchangia ukandamizwaji wa mwanamke kupitia kwa lugha wanayoitumia wanajamii. Ilidhihirika kuwa anayelengwa na sitiari hizi alihitaji uelewa wa mambo ya kitamaduni katika jamii ambapo sitiari hizo zinatumika. Ilieleweka kuwa watumiaji wa sitiari hizi katika muktadha huu wa harusi walipata nafasi ya kuwasilisha hisia na mielekeo yao kulingana na utamaduni wa Abagusii, ambapo hali hii ya mfumodume inajitokeza kupitia kwa majukumu ya kimenke yanayolazimishwa katika jamii. Sawa na msimamo wa Abudi na Yieke (2009), utafiti huu unapendekeza wanajamii wabadilishe ama waache kutumia sitiari zinazomtenga mwanamke. Harakati za mwanamke za kutaka kujikomboa kutoka kwa minyororo ya mfumodume, huchukuliwa kama jambo la kigeni ambalo linaingilia utamaduni wa Kiafrika hasa nafasi ya juu anayotengewa mwanamume. Kutokana na harakati hizo, jamii hutumia njia zozote ili kuzima juhudi hizi za mwanamke. Hata hivyo, mwanamke anastahili kujikomboa kwa kuchukua nafasi zilizotengwa awali kuwa ni za wanaume pekee kama vile za uongozi.

Marejeleo

Aberi, G. & Yieke, F. A. (2009) *Influence of gendered linguistic images on girl education: A case study of southern Kisii district, Kenya.* Unpublished MA thesis, Egerton University, Kenya.

Abudi, M. & Yieke F. A. (2009) *Language, gender and power relations. A case study of sexism in Dholuo Honorific expressions and idioms in the private domain.* Unpublished MA thesis, Egerton University, Kenya.

Betty, F. (1977) *The feminine mystique.* Newyork: Norton and co.

Fairclough, N. (1992) *Discourse and social change.* London: Longman group.

Levine, R. (1980) *Adulthood among the Gusii of kenya.* Cambridge, Massachusetts: Harvard University Press.

Millet, K. (1978) *Sexual politics.* London: Routledge.

Milroy, P. (1987) *Observing and analysing natural language.* London: Basil Blackwell.

Momanyi, C. (2001) Nafasi ya Mwanamke katika Ushairi wa Shabaan Robert. *Jarida la Kiswahili la isimu na fasihi, juzuu 1996/97. Chuo kikuu cha Dar es Salaam*.

Mwosha, F. (2011) Matumizi ya lugha katika sherehe za kumfunda mwari (dhifa za jikoni). *Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta*.

Ndumbu , J. (2013) *Matumizi ya takriri na sitiari katika utenzi wa RASI'LGHULI.* Chuo kikuu cha Nairobi, Kenya.

Nyang'era, N. (1999) *The making of a man and woman under Abagusii customary laws.* Kisii: Dal-rich printers.

Omari, S., Mkomwa , A., & Mlingi, S. (2016) Texts on swahili cultural artefacts in Tanzania and the representation of women's voice. *Journal of University of Namibia Language Centre*, 20.

Onchoke, S. (2017) A cognitive analysis of women metaphors in ekegusii language. Southwest University China.

Otiso, Z. K. (2016) Gender construction, representation, contestation and maintenance. *A case study of Ekegusii discourse.* Unpublished PhD thesis University of Nairobi, Kenya.

Riro, M. (2006) Usawiri wa mwanamume katika nyimbo na nyiso za jando miongoni mwa abakuria. *Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya*.

Rutere, A. (2009) *Women and patriachal power: In the selected Novels of Ngugi wa Thiong'o.* Maryland USA: Black academy Press.

Senkoro, F. (1982) *Fasihi.* Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Steady, F. (1981) *The Black women cross-culturally.* Cambridge: Schenkan Publishing Co. Inc.

TUKI (1990) *TUKI English-Swahili Dictionary.* Dar-es-salaam: Oxford University Press.

van Dijk, T. (1999) *Critical discourse analysis and conversation analysis: Discourse and society.* London: Sage Publications.

Wamitila, K. (2003) *Kamusi ya fasihi istilahi na nadharia.* Nairobi: Focus Publications Ltd.